**BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KUSIMAMIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA KUHUSU RIPOTI YA MWAKA YA TUME YA KUREKEBISHA SHERIA ZANZIBAR, 2021/2022

---

**Mheshimiwa Spika,** awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehma, Muumba wa mbingu na ardhi na vyote vilivyomo ndani yake kwa kutujaalia uzima na afya njema ambayo imetuwezesha kutekeleza vyema majukumu yetu.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati hii, inatoa shukurani zake za dhati kabisa kwa Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kusimamia vyema amani na utulivu nchini na kuhakikisha amani hii imelindwa na kusaidia kukuza uchumi wa nchi yetu. Kwa hakika miongozo na maelekezo yake yamekuwa na tija katika kufanikisha utekelezaji wa shughuli mbali mbali za maendeleo. Tunamuomba Mwenyezi Mungu azidi kumpa uwezo, ujasiri, hekima na busara katika uongozi wake ili azma yake ya kuwatumikia na kuwaletea maendeleo wananchi ikamilike.

**Mheshimiwa Spika,** vile vile, natumia fursa hii, kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kusimama mbele ya Baraza lako tukufu kwa ajili ya

kukidhi matakwa ya kanuni ya *44(3)* ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi, Toleo la *2020* ya kutoa maoni ya Kamati yetu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusiana na **Taarifa ya Serikali juu ya Ripoti ya Mwaka ya Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar.**

**Mheshimiwa Spika,** Ripoti hii imechambua na kueleza kwa ufupi Sheria mbali mbali za Zanzibar ambazo zimeshadumu kwa muda mrefu na zile ambazo zimekuwa na changamoto katika utekelezaji wake licha ya kuwa zimepitishwa katika chombo hiki kwa miaka ya hivi karibuni. Aidha, maoni na ushauri wa Tume ambao umetolewa ndani ya ripoti hii ya mwaka ni muongozo bora katika kuziboresha sheria zetu. Kamati, inaishauri Serikali kuzifanyia kazi sheria zote ambazo zimeainishwa katika kitabu hiki kwani mchango wake ni mkubwa katika kujenga Taifa lililobora na hatma ya kukuwa kwa demokrasia ya Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,** kwa heshima kubwa naomba kuwatambulisha Wajumbe wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Machano Othman Said | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Mtumwa Peya Yussuf | Makamu Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Suleiman Makame Ali | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Salma Mussa Bilal | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Mohammed Mgaza Jecha | Mjumbe |

| | | |
|---|---|---|
| 6. | Mhe. Zaina Abdalla Salum | Mjumbe |
| 7. | Ndg. Ali Alawy Ali | Katibu |
| 8. | Ndg. Mwanaisha Mohammed Kheir | Katibu |
| 9. | Ndg. Amina Abeid Hemed | Mkalimani. |

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yetu ilikutana na kuijadili ripoti hii ya Mwaka mmoja ya Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar na kuipitia ukurasa kwa ukurasa na kutoa maoni yake juu ya kila hatua ambayo imeona ni vyema kufanya hivyo ili kujenga na kufikia dhamira njema ambayo Serikali yetu imekusudia katika kuziboresha sheria zetu.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa dhamira ya Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar ni "Kuzifanyia Mapitio Sheria zote za Zanzibar ili zilingane na muelekeo wa mabadiliko na mahitaji ya kijamii, kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni kwa watu wa Zanzibar." Kamati yangu inaishukuru sana Tume hii kwa kutekelza vyema dhamira yake hii na kuhakikisha kwamba wameweza kuzipitia sheria zote za Zanzibar na kuzibainisha zile zenye mapungufu pamoja na kushauri namna gani ya kufanya ili ziwe bora.

**Mheshimiwa Spika,** kwakuwa ripoti hii imezungumzia sheria mbali mbali ambazo zimetolewa ushauri, hivyo, Kamati yangu haitarejea tena maelezo yalitolewa na Tume kuhusiana na sheria hizo bali Kamati itaongezea tu pale inapopaswa kufanya hivyo. Kwa mnasaba huu, Kamati yangu katika *ukurasa wa 32 na 33* imelezwa kupitia ripoti hii kuwepo kwa mapitio ya sheria ya Jumuiya, Namba 6 ya mwaka 1995 kwa lengo la kwenda

sambamba na sera ya Taasisi zisizo za Serikali (NGO's) ya mwaka 2009 na kuimarika kwa demokrasia nchini. Hapo awali, Kamati hii imewahi kuishauri Serikali kupitia Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalumu za SMZ kuhusu maendeleo ya Taasisi za kiraia na kuitaka ofisi ya Mrajisi kufuatilia kwa kina maendeleo ya Taasisi hizi.

**Mheshimiwa Spika,** ni vyema na ipo haja kwa Asasi za kiraia kuwa na katiba zao na kuhakikisha kazi zote wanazofanya zinaenda kwa mujibu wa katiba hizo. Tukumbuke kwamba hivi karibuni limetokea wimbi la Jumuiya ambazo zinafanya kazi bila kuzingatia katiba zao na katiba ya nchi, hivyo kufanya kazi kwa kupotosha maadili, mila na silka za watanzania walio wengi. Kamati yangu, inaona ipo haja ya Mrajisi kuendelea kuwa na mamlaka kisheria ya kuzifuta Jumuiya ambazo zitakwenda kinyume na Katiba ya Nchi lakini pia watafanyakazi kinyume na malengo yao ambayo yameainishwa kupitia katiba zao wenyewe.

**Mheshimwia Spika,** kwa upande wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Namba 4 ya mwaka 2015 Kamati yangu inaipongeza Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar kwa kuipitia na kutoa maoni ya sheria hii, sheria ambayo imekuwa mara kwa mara ikifanyiwa marekebisho kutokana na utekelezaji wake wa kila siku. Kamati inaunga mkono maoni yaliyotolewa na inazidi kushauri kwamba katika kuweka sharti linalomlinda mtoa taarifa au mlalamikaji dhidi ya mlalamikiwa. Kamati yangu inashauri kuwekwa kifungu cha kutoa adhabu kwa baadhi ya viongozi wanao wachukulia hatua kali zisizostahiki kisheria watumishi ambao wanaripoti katika ofisi za Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma makosa yanafanywa

dhidi yao na viongozi wao kinyume na maadili ya viongozi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imeona katika *ukurasa wa 44* wenye mapitio ya Sheria ya Utumishi wa Umma, Namba 2 ya 2011 maoni na ushauri mbali mbali umetolewa kwa lengo kuifanya sheria hii iwe bora na inayotekelezeka. Kamati inashauri pia kuangaliwa kwa kina suala la likizo ya uzazi kwa watumishi wanawake kwani likizo ya uzazi ilivyo sasa haitoi nafasi ya kutosha kwa akina mama kuwahudumia watoto wao ipasavyo. Aidha, Kamati inashauri sheria hii izingatie pia mazingira ya mama aliyejifungua mtoto njiti (mtoto ambaye hajafika muda wa kawaida wa kuzaliwa) ili aongezewe muda wa likizo ya uzazi kisheria.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yangu licha ya kuwa tumeelezwa kuwa mapitio ya sheria hii yameshapelekwa Serikalini na hatua mbali mbali zinaendelea kwa upande wa Serikali lakini bado ipo haja ya sheria hii kuangaliwa kwa kina suala la nidhamu ya watendaji na kufanyiwa kazi kwa haraka kwani nidhamu ya watendaji wetu wa sekta nyingi za umma imeshuka na hivyo kufanya huduma zinazotolewa kuwa mbovu na kushindwa kufikia malengo ya Taasisi hizo. Kamati inaishauri Serikali kuja na suluhisho la kudumu katika kulinda na kusimamia nidhamu za watumishi ikiwa ni pamoja na kuwekwa taratibu zitakazo punguza umuhali katika maeneo ya kazi hasa kwa watumishi wanaovunja nidhamu na maadili ya kazi kwa kutumia nafasi zao.

**Mheshimiwa Spika,** Sambamba na hayo, katika *ukurasa wa 30 na 31 kamati* imeyapitia kwa umakini mkubwa maoni yaliyotolewa katika mapitio

ya Sheria ya Mfuko wa Jimbo, Namba 4 ya mwaka 2012 na kuyachambua kama yalivyopendekezwa na Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar. Kamati imegundua kuwa changamoto za Sheria hii ni nyingi na utekelezaji wake ni mgumu licha ya kushauriwa kufanywa marekebisho katika sehemu inayoweka masharti ya fedha ili kutoa msamaha wa kutozwa kodi kwa fedha za miradi inayotekelezwa kwenye Jimbo kupitia Mfuko wa Maendeleo wa Jimbo. Kwa kuwa sheria hii imeshafanyiwa kazi siku nyingi pamoja na kupokea maoni mbalimbali ukiwemo ushauri wa waheshimiwa wajumbe wa Baraza hili kuhusu namna bora ya kuboreshwa kwa Mfuko huu, Kamati inaishauri kwamba Serikali ione sasa ipo haja ya kufanyiwa kazi maoni yaliyotolewa kwa uharaka ili sheria hii iweze kutekelezeka kwa urahisi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inashauri Serikali pia, kufikiria kuongeza fedha katika Mfuko huu kwani fedha zinazotolewa sasa ndogo mno hali inayoathiri utekelezaji wa miradi yote ya maendeleo iliyodhamiriwa kufanyika kutokana na kupanda kwa gharama za vifaa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yangu inaishauri Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar kuzipitia sheria za Shirika la Umeme Zanzibar na Sheria ya Mamlaka ya Maji Zanzibar ili kuona kama zinakidhi kutumika katika masuala yote ya sekta ya Nishati na Madini ambapo kwa sasa sekta hizi zinatumia sheria hizo kwa maana kwamba hakuna sheria rasmi ambazo zilizoanzishwa kuendesha sekta hizi za Nishati na Madini.

**Mheshimiwa Spika,** katika ukurasa wa 45 wa ripoti hii imeeleza jukumu lake la kuziweka sheria zetu katika lugha rahisi yaani lugha nyepesi ambazo zinaeleweka na kila mmoja katika jamii. Kwa mnasaba huo, Tume inafanyakazi ya kutoa elimu kwa umma juu ya umuhimu wa kuzifahamu sheria na kuzitekeleza ipasavyo, ili kuhakikisha elimu imemfikia kila mmoja, Kamati inaipongeza Tume kwa kuandaa vitabu ambavyo vitasaidia kufafanua matukio mahususi katika jamii ikiwemo suala la Ndoa na Talaka, suala la Vizazi na Vifo pamoja na suala zima la Usajili wa Mzanzibari Mkaazi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inapenda kuzishauri Taasisi zote zenye kusimamia sheria na kutoa haki kwa jamii kuhakikisha zinatoa elimu ya kutosha kwa raia juu ya matumizi bora ya Sheria. Aidha, kwa upande wa Serikali inashauri kuyafanyia kazi maoni na mapendekezo yanayotolewa na Tume ya Kurekebisha Sheria kwa lengo la kuandaa sheria zilizobora ambazo zitatumia lugha zinazotambulika na wananchi pamoja na kuzifanya utekelezaji wake uwe rahisi na wenye kufahamika. Hali itayopelekea Zanzibar iendelee kuimarisha misingi ya demokrasia kwa kuwa na sheria zenye haki na usawa.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kumalizia, kamati inatoa wito kwa serikali kuzifanyia marekebisho Sheria zote ambazo zinatumika tangu kabla ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar ya mwaka 1964.na inatoa wito kwa taasisi zinazohusika kufuatilia baadhi ya taasisi ambazo zinafanya kazi bili ya kuwa na sheria kwa kuhakikisha wanafanya kila linalowezekana kupata sheria mpya kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa majukumu yao.

**Mwisho Kabisa,** naomba kuwashukuru Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza kwa umakini wakati wote nilipokuwa nikiwasilisha hotuba hii na nawaomba Wajumbe wa Baraza hili kutoa michango yao juu ya Taarifa iliyowasilishwa mbele yetu.

**Mheshimiwa Spika,** Naomba Kuunga Mkono Hoja.

..................................

***(Mhe. Machano Othman Said)***

**Mwenyekiti,**

**Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa,**

**BARAZA LA WAWAKILISHI.**

**ZANZIBAR**